Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Machi

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.04 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz



HALIUZWI

## Wanawake na Maendeleo, Bima ndio Maendeleo!

**Wasiliana nasi** coi@tira.go.tz | **Au tupigie** +255 222 132 537 | **FB, IG, X:** //@tira_tz

# Yaliyomo

01




03





01 Wanawake TIRA Washiriki Kilele Siku ya Wanawake Duniani

03 PAC Yaridhishwa na Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu TIRA Dodoma

05 Waziri Ndumbaro Aipongeza TIRA kwa Usimamizi Makini katika Soko la Bima

07 RC Kihongosi Awataka Watumishi wa Serikali Simiyu Kukinga Mali na Miradi ya Serikali kwa Bima

08 Wadau Wakutana Kuhakiki Maoni ya Kanuni za Bima za Kilimo

10 Ziara ya Kamishna wa Bima: Mkuu wa Mkoa wa Mara Asisitiza Mali za Serikali Kukatiwa Bima

12 TIRA Ana kwa Ana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza

14 Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani: Bima na Wanawake, Bima na Jamii: TIRA Yashiriki Utoaji Elimu

16 Shamrashamra Siku ya Wanawake Duniani: Wanawake TIRA Washiriki Utalii Mbugani

18 Utoaji Elimu ya Bima: TIRA Yashiriki Maadhimisho Miaka 30 ya VETA

20 Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda Awahimiza Wananchi Kutumia Huduma na Bidhaa za Bima

21 "Uwajibikaji Wangu ni Msingi wa Kuinua Ubora wa Elimu na Ufaulu Dodoma"



**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba


TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Machi 2025.





Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# Wanawake TIRA Washiriki Kilele Siku ya Wanawake Duniani




Tarehe 8 machi 2025 Wanawake TIRA wakiongozwa na Naibu Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Khadija Said walishiriki Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani yaliyofanyika jijini Arusha katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan alikuwa Mgeni Rasmi.

Akisoma hotuba yake Rais Samia aliwapongeza wanawake kwa kujitokeza kwa wingi na kusema kuwa hatua hiyo imedhihirisha wao sio tu jeshi kubwa bali ni jeshi madhubuti na la kuaminiwa.

Maadhimisho hayo yalitanguliwa maonesho yaliyofanyika kwa wiki moja ambapo TIRA ilishiriki katika utoaji wa elimu ya bima kwa wananchi pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za kibima.




Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2025


MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA (TIRA)


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2025



# PAC Yaridhishwa na Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu TIRA Dodoma




Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mhe Naghenjwa Kaboyoka (Mb) na wajumbe wa Kamati hiyo walitembelea na kuridhishwa na mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Makao Makuu linalojengwa Jijini Dodoma ambalo hadi sasa limefikia asilimia 85 ambapo Mhe. Kaboyoka ameipongeza TIRA kwa usimamizi mzuri wa ujenzi huo ambao umeonesha ubora wa hali ya juu huku ukikamilika kwa wakati.

Pongezi hizo zilitolewa Machi 13, 2025 wakati Kamati hiyo ilipofanya ziara ya ukaguzi wa jengo hilo.

"Tumeridhishwa na ujenzi wa jengo hili, ubora unaonekana kwa macho na hata mtaalamu wetu upande wa kamati pia ametuhakikishia, hongera Kamishna wa Bima na Menejimenti yote kwa usimamizi mzuri" Amesema Mhe. Kaboyoka.

Mhe. Kaboyoka pia alimpongeza Mkandarasi kwa kukamilisha ujenzi kwa wakati huku ufanisi ukiwa wa hali ya juu na kusema kuwa taifa linajivunia kuwa na wataalamu wazawa ambao hufanya kazi kwa ufanisi na kumtaka Mkandarasi huyo kuendelea kutoa huduma hiyo ya ujenzi kwa ufanisi zaidi na kwamba PAC imetambua kazi kubwa na nzuri iliyofanywa kwenye ujenzi wa jengo la TIRA.







"Kama ambavyo huwa tunapaza sauti kukemea kazi mbovu zinazofanywa na baadhi ya Wakandarasi ndivyo leo tunapaza sauti kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Mkandarasi huyu kwenye jengo hili la TIRA. Ni lazima tuwatie moyo pia wanaofanya vizuri" Alisema Mjumbe wa Kamati ya PAC Mhe. Byabato (Mb).

Nae Mjumbe wa Kamati hiyo Mhe. Mhandisi Isaac Kamwelwe (Mb) alisema kazi iliyofanyika kwenye ujenzi wa jengo hilo ni kubwa na kwamba sehemu iliyobaki ni ya ukamilishaji wa jengo. "Nimezunguka jengo zima na nimejiridhisha bila shaka kuwa kazi iliyofanyika ni nzuri, tunaona thamani ya pesa iliyotumika inaakisi uhalisia wa mradi" Amesema Mhandisi Kamwelwe.

Awali akieleza kuhusu mradi wa ujenzi wa jengo hilo Kamishna wa Bima Tanzani Dkt. Baghayo Saqware amesema Mkandarasi wa ujenzi ni Kampuni ya AMI & VAI Investment Company LTD ambayo ni Kampuni inayomilikiwa na Watanzania na iliyopatikana kwa njia ya ushindani ambapo gharama za ujenzi ni kiasi cha TZS 5.9 bn.
Jengo hilo lililoanza kujengwa rasmi mwezi Februari, 2024 ni la awamu ya kwanza ya ujenzi ambapo linajengwa kwenye ardhi ya ukubwa wa Heka 6.

# Waziri Ndumbaro Aipongeza TIRA kwa Usimamizi Makini katika Soko la Bima




Tarehe 4 Machi 2025, Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro alitembelea banda la TIRA katika maonesho ya huduma na bidhaa mbalimbali yaliyofanyika mkoani Arusha kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake duniani yaliyoadhimishwa tarehe 8 machi 2025 ambapo Waziri aliipongeza Mamlaka kwa kazi nzuri ya utoaji elimu kwa wananchi kuhusu bima.

Aidha, Waziri Ndumbaro alitoa rai kwa TIRA kuendeleza kazi nzuri wanayoifanya ili kukuza soko la bima nchini na kuhakikisha watanzania wengi wanafahamu umuhimu wa bima kujikinga na majanga mbalimbali na kusimamia sheria za bima ipasavyo.

“Nafurahi kuona mpo hapa katika wiki ya wanawake iliyoandaliwa na mkuu wa mkoa wa Arusha Mhe. Paul Makonda, na sisi Wizara yenye dhamana ya haki, Wizara ya Katiba na Sheria tumekuja kuungana nanyi kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi, nawashukuru sana”, alisema.

TIRA ilishiriki maonesho hayo kwa lengo la kufikisha elimu ya bima kwa wananchi mbalimbali, waliotembelea maonesho hayo katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid mjini hapo.


Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
TIRA


Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
TIRA
MAJUKUMU YETU

# RC Kihongosi Awataka Watumishi wa Serikali Simiyu Kukinga Mali na Miradi ya Serikali kwa Bima








Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Kenani Kihongosi alitoa rai kwa watumishi wa umma mkoani humo kutumia fursa kuwekeza kwenye sekta ya bima ili kuondokana na umasikini.

Alisema hayo tarehe 5 Machi, 2025 wakati akifungua mafunzo ya bima kwa watumishi wa Umma mkoani hapo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Mhe. Kihongosi aliwasihi watumishi wa Umma mkoani Simiyu kutumia fursa ya elimu waliyoipata kuwa mawakala ili wajikwamue na umaskini.

Aidha, aliagiza watumishi hao kuchukua hatua ya kuzikatia bima mali na miradi ya Serikali ikiwemo majengo, magari na hata vifaa mbalimbali vya kazi ili kukinga vitu hivyo na majanga yanayoweza kutokea.

Awali, akizungumza katika mafunzo hayo Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alibainisha mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu ya bima kwa watumishi wa umma mkoani hapo kwa kuwahamasisha kuzikinga mali na miradi ya Serikali na kuwaeleza kuhusu fursa mbalimbali zilizopo kwenye Sekta ya Bima ili wawekeze kwa kuwa Mawakala wa Bima na kuongeza wigo wa upatikanaji na usambazaji wa bima kwa ujumla.

Akiitambulisha Mamlaka katika mkutano huo, Meneja wa TIRA Kanda ya Ziwa, Bw. Richard Toyota, amesema Mkoa wa Simiyu umepewa kipaumbele kutokana na ongezeko kubwa la pato ghafi la bima, kutoka Shilingi Milioni 5 mwaka 2022 hadi Milioni 97 mwaka 2023, sawa na mara 19 ya ongezeko. Kwa sasa, mkoa huo una watoa huduma wa bima 13, wakiwemo mawakala 5, benkiwakala 5, wauzaji wa bima kidijitali 2, na kampuni 1 ya bima.

Hii ni fursa nzuri ya kupanua wigo wa huduma za bima na kuhakikisha wanasimiyu wengi zaidi wanapata uelewa kuhusu umuhimu wa bima katika maisha yao na shughuli zao za kiuchumi.

# Wadau Wakutana Kuhakiki Maoni ya Kanuni za Bima za Kilimo



Tarehe 28 Machi 2025 katika hoteli ya Ramda jijini Dar es Salaam, Mamlaka ya Umamizi wa Bima kupitia Kurugenzi ya Mipango na Uendelezaji Soko Iliandaa Semina ya uhakiki kutoka kwa wadau kuhusu "Kanuni za Bima ya Kilimo, 2025".

Lengo la semina hii lilikuwa ni kupokea, kujadili na kuhuisha maoni ya wadau ili kuboresha rasimu ya kanuni zinazopendekezwa kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa bima ya kilimo yenye uwazi, ufanisi na uwajibikaji nchini Tanzania.

Semina hiyo iliyofadhiliwa na UNDP ilihudhuriwa pia na Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware pamoja na Naibu Kamishna wa Bima Bi. Khadija Said ilikutanisha Wadau wengine wanaojihusisha na Bima za kilimo ikiwemo pia Watafiti, Kampuni za bima, taasisi za kifedha, wawakilishi wa serikali, na washirika wa maendeleo.

Wakati wa hotuba yake, Dkt. Baghayo Saqware alieleza kuwa Serikali ina matumaini makubwa ya kuona Skimu ya Bima ya Kilimo (TAIS) ikitekelezwa kwa mafanikio, ili kuiwezesha sekta ya kilimo ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa, kupata kinga madhubuti dhidi ya majanga mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, wakulima na wananchi kwa ujumla watanufaika kwa kupata tija zaidi kupitia kilimo chenye uhakika na





endelevu.

Aidha, Dkt. Saqware alibainisha kuwa kupitia kanuni hizi, Serikali inalenga kuwawezesha wakulima, hususan wakulima wadogo, kupata huduma za bima ya kilimo kwa gharama nafuu, zenye ubora na zinazokidhi mahitaji yao halisi. Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji, kuimarisha ustahimilivu wa wakulima dhidi ya athari za majanga mbalimbali, pamoja na kuvutia uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya kilimo.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said, katika hotuba yake ya kufunga kikao hicho aliwataka wadau kuendelea kushiriki katika hatua zinazofuata ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kanuni hizo.

Alisema: “Majadiliano ya leo yameonesha kwa dhahiri umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria utakaohakikisha malengo tarajiwa ya upatikanaji wa bima za kilimo nchini yanafikiwa.

Maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika kikao hiki yatakuwa msingi wa kuboresha rasimu ya kanuni hizi ili kuweka mazingira bora kwa ukuaji wa bima za kilimo hapa nchini.”

Aidha, aliwasihi wadau kuendelea kushiriki kikamilifu katika hatua za utekelezaji wa kanuni hizo na kuunga mkono juhudi za Serikali za kuweka mfumo thabiti wa utoaji na upatikanaji wa bidhaa na huduma za bima zinazogusa maisha ya wananchi wengi.

# Ziara ya Kamishna wa Bima: Mkuu wa Mkoa wa Mara Asisitiza Mali za Serikali Kukatiwa Bima



yanayoweza kutokea. Ameyasema hayo Machi 4, 2025 wakati Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilipofanya ziara ya utoaji elimu ya bima kwa watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara na wajumbe wa Bodi ya Barabara wa mkoa huo katika ukumbi wa uwekezaji wa mkoani hapo

“Hili suala la bima kwa mali za Serikali ni muhimu sana, majengo, magari na mali nyingine za Serikali zinapopata ajali inakuwa ni hasara kubwa kwa Serikali na mara nyingi zinakuwa hazitumiki tena” alisema Mhe. Mtambi.

Akiendelea kuzungumza katika ufunguzi wa kikao hicho Mhe. Mtambi alisema, bima kama ya kilimo inaweza kuwasaidia wananchi wengi kuwekeza kwenye kilimo wakiwa na uhakika wa kupata mazao hata kama msimu huo kilimo kikiwa sio kizuri baada ya kukata bima ya kilimo. “Hii bima ya kilimo ni muhimu sana kwani wananchi wengi wanapata hasara kubwa baada ya kuwekeza na kupata majanga mbalimbali jambo ambalo mkulima huyo akiwa na bima linaepukika”

Awali, akiongoza kikao cha mafunzo ya watumishi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Bw. Gerald Kusaya aliishukuru TIRA kwa kutoa elimu ya bima kwa watumishi na kuwataka watumishi kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwekeza katika masuala ya bima. “Hii ni fursa nzuri kwa watumishi ambayo itawawezesha kuwa wateja wa bima mbalimbali zilizopo hapa nchini pamoja na kuwa wawekezaji katika sekta hii ya bima hata kama bado unaendelea na kazi yako” alisema Bwana Kusaya.

Kwa upande wake, Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alitoa rai kwa watumishi wa Serikali na viongozi kutoa ushirikiano ili kuweza kufanikisha malengo ya Serikali katika kuhakikisha asilimia 50 ya wananchi wanakuwa na bima.

Dkt. Saqware pia aliwasihi viongozi wa Serikali kuona umuhimu wa mali za Serikali zilizopo kwenye maeneo wanayoyasimamia zinawekewa kinga ya kibima ili kuiepushia Serikali hasara inayoweza kutokea inapotokea majanga.

Aidha, Dkt. Saqware amesema TIRA inatoa huduma ya ushauri katika masuala ya bima kwa mali na miradi ya Serikali na kuwahakikishia viongozi kuwa TIRA itatoa ushirikiano kama itaombwa ushauri kuhusiana na masuala ya bima. Dkt. Saqware alieleza TIRA kwa mujibu wa sheria inayo majukumu ya kutoa leseni na kusajili kampuni za bima, kuhakikisha soko la bima ni himilivu na endelevu, kulinda haki za wateja wa bima pamoja na kutoa elimu ya bima kwa wananchi.





# TIRA Ana kwa Ana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza

Ujumbe kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ukiongozwa na Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware wamekutana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda na Katibu Tawala wa mkoa huo, Bw. Balandya Elikana wakati wa mfululizo wa ziara ya elimu ya bima Machi 3, 2025.

Ziara hio ililenga kuhamasisha wakuu wa mikoa, makatibu tawala na watumishi wa umma kuhusu umuhimu wa bima, kuwahamasisha watumishi wa umma kuhusu fursa za kuwekeza zilizopo katika sekta ya bima na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.












NORTHERN ZONE OF







# Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani: Bima na Wanawake, Bima na Jamii: TIRA Yashiriki Utoaji Elimu



Siku ya wanawake duniani iliadhimishwa rasmi kitaifa tarehe 8 Machi 2025, jijini Arusha ambapo ilitanguliwa na maonesho ya huduma na bidhaa mbalimbali yaliyoanza tarehe 1 – 8 machi 2025, maadhimisho hayo yalifanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini hapo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilishiriki maonesho hayo kama sehemu ya kufikisha elimu ya bima kwa wanawake washiriki na jamii kwa ujumla.  Mamlaka ilitoa elimu kwa umma, kusikiliza changamoto mbalimbali za kibima na kutoa majibu kwa maswali yaliyoulizwa na wadau kuhusu bima.

Moja, ya mambo muhimu yaliyoulizwa ni pamoja na wananchi kutaka kufahamu kuhusu fursa mbalimbali zilizopo katika soko la bima ikiwemo kuwa wakala wa bima ambapo wataalamu wa bima kutoka Mamlaka walitoa elimu hiyo na kuwahimiza wananchi kujiunga na fursa hizo.

Washiriki pia walielezwa umuhimu wa bima katika kulinda mali afya na

uwekezaji, ambapo walisisitizwa umuhimu wa kukata bima za nyumba, vyombo vya moto, bima za afya,bima za kilimo na ufugaji, bima kulinda biashara, bima ya maisha na nyinginezo.

Maonesho pia yamekuwa ya manufaa kwa wadau wenye changamoto za kibima ambapo wamesikilizwa na kupewa utaratibu sahihi mathalani wa kudai fidia ya madai ya bima na madai yao kurekodiwa kwa ufatiliwaji zaidi.

Maonesho hayo yalibeba kauli mbiu ya "Wanawake na wasichana 2025: tuimarishe haki, usawa na uwezeshaji".





# Shamrashamra Siku ya Wanawake Duniani: Wanawake TIRA Washiriki Utalii Mbugani



Machi 7, 2025 wanawake kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) waliungana na wanawake wengine kutoka taasisi za serikali na binafsi kufanya utalii wa ndani kwa kutembelea mbuga ya wanyama ya Ngorongoro iliyopo mkoani Arusha ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Arusha tarehe 8 machi 2025.

Safari ya tarkibani kilometa 170 ilianzia jijini Arusha hadi wilayani Ngorongoro katika hifadhi hiyo ambapo wanawake hao walipata fursa ya kuona mandhari za kuvutia zikiwemo ziwa, mabwawa, ndege na wanyama mbalimbali kama simba, tembo, nyati na nyumbu. Ikiwa kama kumbukumbu isiyosahaulika katika kusherehekea siku ya wanawake kwa mwaka 2025.

Aidha, maadhimisho hayo pia yalitanguliwa na maonesho ya bidhaa yaliyofanyika kwa siku saba ambapo Mamlaka ilishiriki kwa kutoa elimu ya bima kwa wananchi wa Arusha na maeneo ya jirani.

Siku ya wanawake duniani husherehekewa kutambua umuhimu wao katika jamii, ujumuishi katika maeneo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa lakini pia utetezi wa haki zao na kutobaguliwa kwa jinsia yao.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "wanawake na wasichana 2025: tuimarishe haki, usawa na uwezeshaji".











# Utoaji Elimu ya Bima: TIRA Yashiriki Maadhimisho Miaka 30 ya VETA




Katika kuunga mkono shughuli mbalimbali zinazofanywa na Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA), TIRA ilishiriki maonesho yaliyoandaliwa na chuo hicho kutoa elimu ya bima kwa umma ambayo yalifanyika katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere Dar es Salaam kuanzia tarehe 18 - 21 machi 2025.

VETA iliadhimisha miaka thelathini (30) tangu kuanzishwa kwake ambapo maadhimisho hayo yaliambatana na maonesho ya huduma na bidhaa kutoka taasisi za serikali na yalifunguliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Tanzania Dkt. Kassim Majaliwa tarehe 18 machi 2025 na ameipongeza VETA kwa tukio hilo muhimu.
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilishiriki maonesho hayo kwa siku zote nne lengo likiwa kutoa elimu ya bima kwa kuwaelimisha wananchi majukumu yake, umuhimu wa kutumia bidhaa za bima za kawaida na za maisha lakini pia kueleza fursa zilizopo katika sekta ya bima nchini.


MAMLAKA YA USIMAMIZI
WA BIMA TANZANIA






MAMLAKA YA
USIMAMIZI
WA BIMA
TANZANIA
(TIRA)
AKA YA USIMAMIZI
A TANZANIA - TIRA

# Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda Awahimiza Wananchi Kutumia Huduma na Bidhaa za Bima




Machi 20 2025, Waziri Mkuu Mstaafu wa Tanzania, Mhe. Mizengo Pinda alitoa rai kwa watanzania kutumia huduma na bidhaa za bima na kutosubiri hadi pale majanga yanapotokea.

Mhe. Pinda aliyasema hayo alipotembelea banda la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika maadhimisho ya miaka 30 ya VETA yanayofanyika katika ukumbi wa JNICC jijini Dar es Salaam yaliyoanza tarehe 18 machi hadi 21 machi 2025.

Aidha Waziri Mkuu huyo mstaafu alisisitiza elimu ya bima itolewe zaidi kwa wananchi wa mjini na vijijini ili kuongeza idadi ya wanaofahamu kuhusu bima na hatimaye kutumia na kuhamasisha wengine ili kuweza kulinda afya, mali na uwekezaji.

Kwa siku nne TIRA ilishiriki maadhimisho hayo kwa kutoa elimu na kusikiliza maoni mbalimbali yanayotolewa na wananchi wanaotembelea banda lao. TIRA imekuwa ikishirikiana na VETA katika mambo mbalimbali ya utoaji elimu na uhamasishaji wa matumizi ya bima nchini.

# ’Uwajibikaji Wangu ni Msingi wa Kuinua Ubora wa Elimu na Ufaulu Dodoma”



Kauli mbiu hii ilitekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushiriki na kudhamini tuzo katika Mkutano wa Wadau wa Elimu ulioandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Bi. Rosemary Sitaki Sinyamule tarehe 20 Machi 2025 ukiwa na lengo la kutunuku tuzo kwa walimu, wanafunzi, shule na wilaya, zilizofanya vizuri katika mitihani ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita kwa mwaka 2024 katika mkoa wa Dodoma.

Tuzo hizo zimekuwa hamasa kubwa kwa wale wote waliofanya vizuri kwani zilifurahiwa na pia kuwa chachu kwa wengine katika kuhakikisha wanaongeza bidii katika mitihani yao na hivyo kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kwa ngazi za wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla ambapo sekta ya elimu nayo itazidi kuwa bora. Katika Mkutano huo uliohudhuriwa na wadau mbalimbali wa elimu zaidi ya elfu mbili, Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo A. Saqware alipata nafasi ya kueleza majukumu ya Mamlaka pamoja na manufaa ya bima.

Kamishna Saqware aliwaeleza wadau hao mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwamba walimu, wanafunzi na wananchi wote wakate bima kwa ajili ya kulinda afya zao, kulinda mali zao na za Serikali kwa ujumla. Lakini pia aliwahamasisha wadau hao kuwa bima ni sehemu ya kujiongezea kipato kwa kuwa wakala wa bima.

Mgeni Rasmi wa Mkutano huo alikuwa Dkt. Doto Mashaka Biteko ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Bi. Rosemary Sitaki Sinyamule.











# Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

*Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara*

## Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

## Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

## Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

## Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

## Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

## Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

## Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

## Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

## Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

## Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

## Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

## Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

## Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

## Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

## Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa

viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

## Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

## Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za umachinga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.

# Tupo nchi nzima!

## Makao Makuu Dodoma, Ofisi ya Zanzibar, Ofisi ya Dar es Salaam pamoja na Ofisi za Kanda

| Kanda | Mkoa |
|---|---|
| **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** | Mbeya, Njombe na Songwe |
| **Kanda ya Kaskazini** | Arusha, Kilimanjaro na Tanga |
| **Kanda ya Ziwa** | Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu na Geita |
| **Kanda ya Mashariki** | Dar es Salaam, Pwani na Morogoro |
| **Kanda ya Kati** | Dodoma, Manyara na Iringa |
| **Kanda ya Magharibi** | Tabora, Shinyanga na Singida |
| **Kanda ya Kusini** | Lindi, Mtwara na Ruvuma |
| **Kanda ya Ziwa Tanganyika** | Katavi, Rukwa na Kigoma |
| **Kanda ya Unguja** | Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi - Chakechake |
| **Kanda ya Pemba** | Kaskazini Pemba na Kusini Pemba - Wilaya ya Kati |


**TIRA - Kwa soko salama la Bima**

# Matukio kwenye Vibango




Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
Miaka Minne
ya Rais Samia
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inakupongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miaka minne ya uongozi wako mahiri.
Hongera kwa kuendelea kuchangia ustawi wa wananchi na uchumi wa taifa.
TIRA iko pamoja nawe katika kujenga Tanzania yenye maendeleo endelevu.


Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
Mkutano
wa Wadau wa Elimu
2025
MGENI RASMI
Mhe. Dkt Dotto Biteko (Mb)
Naibu Waziri Mkuu
TIRA Tunashiriki


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
Heri ya Siku ya
WANAWAKE
Duniani
Machi 8, 2025
TIRA KWA SOKO SALAMA LA BIMA
@tira_tz
www.tira.go.tz


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
Mwanamke nguzo ya familia tumia huduma za Bima kuikingia familia yako na majanga na kuimarisha ustawi wake
Mhandisi Zena Ahmed Said
TIRA KWA SOKO SALAMA LA BIMA
@tira_tz
www.tira.go.tz


Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)
Ramadan
kareem


MAMLAKA YA USIMAMIZI
WA BIMA TANZANIA (TIRA)
Kuelekea Maadhimisho ya Siku ya
Wanawake Duniani
Bi. Khadija Said
+255 022 213 2537
www.tira.go.tz
tira_tz



# TIRA & 2025

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz